**BARUA YA HISA STAHILI (PROVISIONAL ALOTMENT LETTER – PAL)**

Mkurugenzi Mkuu
CRDB Bank Plc
Gorofa ya Nne (4)
Office Accommodation Scheme Building, Mtaa wa Azikiwe
S. L.P. 268
**Dar-es-Salaam**

**YAH: TOLEO LA HISA STAHILI 435,306,432 ZA KAWAIDA ZA CRDB BANK PLC KWA BEI YA SHILINGI 350 KILA HISA LIKUBALIKE KABLA YA SIKU YA ALHAMISI TAREHE 16 JULAI, 2015**

Mpendwa Mwanahisa,

**Mgawo wa Awali**

Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB wamekupatia mgawo wa awali wa idadi ya Hisa za kawaida zinazooneshwa kwenye ukurasa wa kwanza wa fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form), ikiwa ni Hisa moja (1) mpya kwa kila Hisa tano (5) za kawaida unazomiliki kama zinavyoonekana kwenye rejesta ya wanahisa wa Benki tarehe 18 Juni 2015 (Record date).

Hisa mpya zitakazotolewa zitakuwa na hadhi sawa na Hisa za kawaida za Benki ya CRDB zilizopo sasa, ikiwa ni pamoja na kupata gawio lolote na michango mingine yoyote itakayotolewa, kutangazwa, kufanyika au kulipwa kwa Hisa za kawaida kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Desemba, 2015.

Unaweza kukubali hisa zote mpya kama ulivyogawiwa, kukubali kiasi au kutochukua Hisa zote. Wanahisa watakaokubali kuchukua hisa zote watatakiwa kujaza sehemu A(i) ya fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form), wakati watakaochukua kiasi na kukataa Hisa zilizobaki watatakiwa kujaza sehemu A(ii) ya fomu. Wale watakaokataa kutumia haki yao watatakiwa kujaza sehemu B (i).

**Kukubali Kuchukua Hisa Zote**

Kama umeamua kuchukua Hisa zote kama ulivyogawiwa, tafadhali jaza sehemu ya fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form) iliyoambatanishwa. Fomu iliyojazwa kwa ukamilifu pamoja na pesa taslim, hundi binafsi au hundi ya benki yenye kiasi kinachotakiwa kulipwa lazima vikabidhiwe kwa wakala yeyote wa Toleo sio zaidi ya siku ya Alhamisi tarehe 16 Julai, 2015 (wakala wa Toleo wameorodheshwa ukurasa namba 46 wa Waraka Huo). Hundi ni lazima ziandikwe kwa kumlipa wakala wa upokeaji fedha. Hundi zote zitapelekwa benki mara zinapopokelewa na fomu zilizoambatanishwa na hundi ambazo zimerudishwa bila kulipwa, fomu hizo zitakataliwa na kurudishwa kwa wenyewe kwa njia ya posta.

**Kuchukua Baadhi ya Hisa**

Kukubali kuchukua baadhi ya Hisa, tafadhali jaza namba (ii) ya sehemu A na wasilisha fomu yako ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form) pamoja na pesa taslim au hundi ya malipo kwa wakala yeyote wa upokeaji malipo kiasi chote kinacholipwa kulingana na idadi ya Hisa ulizoamua kuchukua (wakala wa Toleo wameorodheshwa ukurasa namba 46 wa Waraka Huo).

**Manunuzi na Mauzo ya Haki Stahili**

Kibali cha kufanya mauzo na manunuzi ya Haki stahili kimetolewa na Soko la Hisa. Hivyo miamala ya Haki stahili itafanyika kati ya tarehe 26 Juni, 2015 na tarehe 16 Julai, 2015. Mdhamini Mwekezaji ananunua Haki stahili kwa bei ya shilingi 32 kila Hisa mpya kwa kuzingatia ukomo wa wajibu wa udhamini na malipo yatafanywa katika kipindi cha wiki nne (4) baada ya kufungwa kwa Toleo. Kwa hiari yao, wanahisa stahili wanaweza kuamua kutofanya chochote, hivyo haki zao kuuzwa kwa Mdhamini Mwekezaji.

**Mgawo wa Hisa za Ziada**

Wanahisa wote watakaoomba Hisa zao mpya zote watapokea idadi kamili ya Hisa mpya kama zinavyoonekana kwenye fomu zao za mgawo wa awali (PAL). Hisa mpya ambazo hazitochukuliwa zitahesabika kama haki ambayo haikutumika na zitauzwa kwa Mdhamini Mwekezaji kwa shilingi 32 kwa kila Hisa mpya (kuzingatia ukomo wa wajibu wa udhamini).

**Kukubali na Kulipa**

Stakabadhi ya malipo pamoja na fomu ya Hisa stahili iliyosainiwa ndio itathibitisha kukubali kununua Hisa stahili zote au sehemu ya Hisa stahili kama ilivyo ainishwa katika barua hii. Mwanahisa anaye kidhi vigezo ana uhuru wa kuchukua Hisa stahili zote, kwa sehemu au kutochukua kabisa. Mwanahisa anayekidhi vigezo endapo ataamua kuchukua hisa zote atatakiwa kuzingatia utaratibu ufuatao:

i) Ukikubali kununua Hisa stahili na kujaza fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form), haiwezekani kubadilisha uamuzi.

ii) Wale wanaotaka kuomba Hisa mpya lazima wajaze kwa ukamilifu fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form).

iii) Isipokuwa kwa uzembe au kukosea kwa upande wa Benki, washauri wake au wakala yoyote aliyekubalika, vinginevyo wote hawa hawatawajibika endapo fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form) haitawasilishwa hadi tarehe ya mwisho ya kupokea maombi.


iv) Fomu inayoonyesha kuwa Mwanahisa amekubali inaweza kuwasilishwa kwa kujaza fomu husika pamoja na kulipa ada ya maombi kwa idadi ya Hisa zinazoombwa, baada ya hapo haiwezi kuahirishwa. Fomu hii ikiwa imekamilika ni makubaliano kamili kisheria, kwa idadi ya Hisa mpya zilizoombwa, kama inavyoonyeshwa kwenye fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form). Fomu hii ni lazima isainiwe ili kukidhi matakwa ya kisheria.

v) Fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form) iliyosainiwa na kujazwa vizuri, ni lazima iwasilishwe Benki ya CRDB moja kwa moja au kwa kupitia kwa wakala aliyeidhinishwa pamoja na malipo kulingana na idadi ya Hisa stahili zilizotolewa. Malipo haya lazima yafanyike kama ilivyoelekezwa katika Waraka wa Maelezo yaani kabla ya saa kumi jioni siku ya Alhamisi tarehe 16 Julai, 2015. Tofauti na hapo itachukuliwa kuwa mgawo wa awali umekataliwa na kufutwa.

vi) Benki imechukua wajibu wa kuwalipa kwa jumla wanahisa ambao hawakuzichukua Haki stahili zao katika kipindi kisichozidi wiki nne (4) baada ya kufungwa kwa Toleo.

Naambatanisha fomu ya Kukubali na kuchukua Hisa Stahili (Entitlement and Acceptance Form) pamoja na mwongozo wa maombi.

Wenu Mtiifu,



Martin J Mmari

**Mwenyekiti wa Bodi**